

JARIDA LA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO



Wizara ya Furaha

Toleo Maalum la: 14 | 23 Juni, 2021 | www.habari.go.tz

MICHEZO UMISSETA 2021 YAWAPA JUKWAA WASICHANA



Wizara HabariTz



Wizara_habaritz



Wizara_HabariTZ



**YALIYOJIRI KATIKA
WA MASHINDANO YA
MICHEZO YA UMISSETA
23 Juni, 2021**

**KAULIMBIU: "MICHEZO SANAA NA
TAALUMA KWA MAENDELEO YA
UCHUMI WA VIWANDA"**

NUKUU YA WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI – SMZ MHE. RAHMA KASSIM ALLY



Ninawatakia mashindano mema katika mechi yenu, kila mmoja wenu anuie kushinda.

Ila baada ya mchezo wote muwe kitu kimoja maana michezo ni upendo.

Michezo itusaidie kuimarisha muungano wetu.

MHE. RAHMA KASSIM ALLY

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano
na Uchukuzi – SMZ**



WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI – SMZ
MHE. RAHMA KASSIM ALLY AKIKAGUA TIMU ZA MPIRA WA MIGUU
PEMBA NA SONGWE KABLA YA KUANZA PAMBANO.



TIMU YA PEMBA



TIMU YA MKOA WA SONGWE

NUKUU YA DKT. EMMANUEL ISHENGOMA MKURUGENZI WA IDARA YA MAENDELEO YA SANAA – WHUSM



Mashindano ya UMISSETA upande wa Sanaa za Maonesho yanaanza leo 23 Juni, 2021 kwa Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar kushindana katika Kwaya na Ngoma.

Aidha, tofauti na ilivyokuwa wakati wa UMITASHUMTA, mashindano upande wa Kwaya na Ngoma yanafanyika mchana katika ukumbi wa Benjamin Mkapa chuo cha Mtwara TTC Kawaida sambamba na mashindano ya michezo mingine ili kutoa fursa kwa viongozi, wanafunzi na wenyeji wa Mkoa wa Mtwara kujionea vipaji vya vijana wetu.

DKT. EMMANUEL ISHENGOMA

**Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya
Sanaa – WHUSM**



MCHEZAJI WA SIKU

MSHIRIKI ANATORIA AUDAX AMBAYE NI GOLIKIPA KUTOKA MKOA WA KAGERA NDIO MCHEZAJI WA SIKU. AMEONESHA UMAHIRI WA HALI YA JUU KUTOKANA NA UWEZO WAKE WA KIPEKEE WA KUZUIA MAGOLI.





Namshukuru Mungu anayenipa nguvu kila siku ya kuisogelea ndoto yangu ya kuwa golikipa wa kudaka kwenye mashindano ya dunia kwenye soka la wanawake.

Leo nimeokoa magoli mengi sana katika mechi hii.

Kipekee namshukuru Rais wetu mpendwa Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa kipaombeke sisi watoto wa kike kwenye michezo.

Tunamuahidi hatutamuangusha.

ANATORIA AUDAX

Golikipa namba 1

Timu ya soka wasichana - KAGERA

MPIRA WA WAVU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA WAVU UPANDE WA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 23, 2021. TIMU ZA MIKOA YA ARUSHA 3 (WENYE PINKI) NA RUVUMA O (WENYE NYEKUNDU).



MPIRA WA WAVU WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA WAVU UPANDE WA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 23, 2021. TIMU ZA MIKOA YA KILIMANJRO O (WENYE BLUU) NA MARA 3 (WENYE BLUU NA MISTARI).



MPIRA WA KIKAPU WASAICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU UPANDE
WA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 23, 2021. TIMU
ZA MIKOA YA LINDI 19 (WENYE BLUU BAHARI) NA
GEITA 27 (WENYE KIJANI).



MPIRA WA KIKAPU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU UPANDE
WA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 23, 2021. TIMU
ZA MIKOA YA SONGWE 13 (WENYE NYEUPE) NA
MBEYA33 (WENYE NYEKUNDU).



SANAA ZA NDANI KWAYA

MASHINDANO YA UMISSETA UPANDE WA SANAA ZA NDANI
(KWAYA) YAANZA RASMI LEO, JUNI 23, 2021. MIKOA
ILIYOANZA LEO NI TANGA, SHINYANGA, RUKWA NA
ARUSHA.



TANGA



SHINYANGA



RUKWA



ARUSHA

MPIRA WA PETE

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA PETE
YAMEENDELEA LEO, JUNI 23, 2021. TIMU ZA MIKOA YA
GEITA 18 (WENYE KIJANI) NA SONGWE 32 (WENYE
BLUU).



MPIRA WA PETE

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA PETE
YAMEENDELEA LEO, JUNI 23, 2021. TIMU ZA MIKOA YA
DAR ES SALAAM 37 (WENYE BLUU BAHARI) NA RUVUMA
9 (WENYE BLUU).



MPIRA WA MIGUU WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIGUU KWA
WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 23, 2021. TIMU ZA
YA DAR ES SALAAM 2 (WENYE KIJANI) NA
SIMIYU 1 (WENYE NJANO).



MPIRA WA MIGUU WAVULANA

**MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIGUU KWA
WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 23, 2021. TIMU ZA
YA PEMBA O (WENYE KIJANI) NA
SONGWE 1 (WENYE NYEKUNDU).**



UNITASHUMTA | UMISSETA 2021



#MwakaWaVipaji

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
S.L.P 25, 40470 DODOMA, TANZANIA